# LEARNING BY EAR
# "WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA"

## KIPINDI CHA PILI:" ELIMU NA MAPUUZA"

**MWANDISHI: CHRISPIN MWAKIDEU**
**MHARIRI: ANDREA SCHMIDT**
**MHARIRI MSAIDIZI: Katrin Ogunsade**
**MTAALAM WA AFYA: Dr. Heidrun Hübner**

**Wahusika katika kipindi cha pili:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO(14)
- ZAWADI (INFANT, no actor needed)Mtoto mchanga
- HEADTEACHER(38)/Mwalimu Mkuu
- DAVID(14)
- Narrator/Intro-Outro (same voice)/Msimulizi

**INKISIRI/MSIMULIZI:**

Hujambo msikilizaji na karibu tena katika kipindi hiki cha Noa Bongo Jenga Maisha yako ikiwa leo tunaingia kwenye sehemu ya pili ya mchezo wa radio kwa jina **"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA-NI VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA"**. katika sehemu ya kwanza, betina alipelekwa haraka hospitali na akajifungua mtoto wa kiume- zawadi! karembo akiwa nyumbani, alijifunza kuhusu malaria kupitia redio.. alikuwa na hamu mno mpaka akasahau kazi zake za shule. jiunge nasi leo tukijaribu kuchunguza ni yapi yatakayotokea hivi punde. katika makala ya " **ELIMU NA MAPUUZA"**

**MUSIC INTERLUDE**

**SCENE ONE:HEADTEACHER'S OFFICE**

**ASFX: KNOCKS HEARD ON THE DOOR..**

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | **H/TEACHER:** | Karibu..Ingia! (**KWA SAUTI YA JUU)** |
| 2. | **KAREMBO:** | Hujambo Mwalimu?… |
| 3. | **H/TEACHER:** | Sijambo karembo. Nimesikia habari za utatanishi kutoka kwa mwalimu wako wa hesabu kuwa hukumaliza kazi yako ya shule.. karembo! Hata kama wewe ni mwanafunzi wetu bora mwaka huu.. nisikize! Tena yakuingie masikioni |

barabara! Ni lazima ufanye kazi unazopewa na waalimu! Umesikia?

**4.** **KAREMBO:** (**AKIMRAI)** Mwalimu Mkuu..si kwa kupenda..ni vile..

5. **H/TEACHER:** (**KWA UKAKAMAVU)** Kimya!,Karembo,fanya kazi zako kama unavyoambiwa! Usiwe kimumunye kutaka kuharibikia ukubwani! Umekuwa mwanafunzi mzuri siku za nyuma kwanini unataka kuzembea hivi sasa?!

6. **KAREMBO:** (**AKIHUZUNIKA)** Mwalimu niwie radhi…haikuwa nia yangu.. mambo mengi yalitokea jana usiku nyumbani kwetu..kwanza,hatukuwa na mafuta ya taa, pili, mamangu alipelekwa hospitali usiku huo huo mmoja.. na pia…

7. **H/TEACHER:** **(AKIVUTIWA)** Ati mamako? Kulitokea nini? Anajihisi vipi hivi sasa?

**8.** **KAREMBO:** Kwa kweli hatujaonana lakini natumai ni

mzima.. alijifunguwa mtoto wa kivulana anaitwa zawadi.. sasa nina kakangu mdogo!(**KWA FURAHA)**

9. **H/TEACHER:** Hizo ni habari njema! wape pongezi mamako na babako urudipo nyumbani..lakini yote hayo hayajakupa fursa ya kutofanya kazi zako za shule…

10. **KAREMBO:** Bila kukuficha mwalimu… nilifazaika kwa furaha na kusahau kumaliza kazi zangu za shule. Samahani.. sitarudia..

11. **H/TEACHER:** Nafurahi kwa kutonidanganya… lakini radhi yangu haitakupeleka shule bora mwakani! Kweli uongo?

12. **KAREMBO:** Kweli Mwalimu..

13. **H/TEACHER:** Swadakta! jitihada, nidhamu na azimio bora ndiyo yatakayokupa alama nzuri… walimu wote wanatarajia upite kwa alama nzuri! Usituvunje mioyo mwakani… na muhimu zaidi.. usijivunje moyo!! Leo nitakusamehe lakini ni lazima umalize kazi uliyopewa…

14. **KAREMBO:** **(AKISHUKURU)**
Asante mwalimu… mwalimu nataka kukuuliza swali…

**15. H/TEACHER:** Enhe,haya uliza ndio kusudi letu kuwa hapa shuleni**.**

16. **KAREMBO:** Mtu anahitaji kuumwa mara ngapi na mbu anoflesi ili kuweza kupata malaria?

17. **H/TEACHER:** **(BEWILDERED )**
Eti nini?

18. **KAREMBO:** Nilitaka kujuwa ni mara ngapi unapoumwa na mbu..

**19. H/TEACHER:** Nimekusikia ... unataka kunipima werevu wangu... karembo? Ulijuwaje kumuhusu mbu anoflesi.... hatufunzi chochote kuhusu anoflesi katika silabasi yetu...

20. **KAREMBO:** (**SCARED SHE HAS MADE THINGS WORSE)**
nilisikia redioni jana.. na nikahofia kuhusu uhai wa mtoto wetu mchanga na familia yangu pia... unajuwa nyumba yetu imepakana na mto na kuna mbu wengi

mno...

21. **H/TEACHER:** Kwani hamujifuniki kwa neti munapolala?

22. **KAREMBO:** Hapana, baba alisema hawezi kununua..

23. **H/TEACHER:** hawezi kununuwa? Nanialimueleza kuwa zinauzwa? Neti hizi zinatolewa bure! Bila ya hata peni na serikali!na iwapo zinauzwa basi labda kwa senti chache.. kitu muhimu ni kuwa neti hizi huwa zinatibiwa dhidi ya mashambulizi ya mbu...mbu anapoikaribia tu! Anakufa kwa ajili ya dawa hiyo... kwa hivyo zina kinga kina mama waja wazito na watoto wachanga.. ukimtembelea mamako muulize ahimize kutumia neti iliyotibiwa.. swali lako la kuumwa mara ngapi, nitakujibu baadaye....

**NARRATOR:** Basi baada ya hayo malumbano.. mwalimu mkuu alimfurusha karembo. Naye alifanya kazi zake haraka haraka huku akisubiri kengele ya mwisho ipigwe ili akimbilie kumuona mamake na kakake mdogo huko hospitali.Kengele ilipopigwa tu..

**<u>SCENE TWO: DAVID AND KAREMBO AFTER SCHOOL</u>**

**B-SFX: SCHOOL BELL RINGS… SCHOOL CHILDREN'S VOICES TALKING/SHOUTING ETC.**

24. **DAVID:** **(CALLING OUT)**
Karembo!!!!! Ningonje! Mbona waniacha na twaenda sote njia moja?

25. **KAREMBO:** La! David.. leo hatuta andamana mimi naenda hospitali kumuona mamangu na kakangu mdogo... ( FURAHA)

26. **DAVID:** Shabash! Hivyo ni vizuri! Naweza kuja? sijawahi kuona mtoto mchanga...

27. **KAREMBO:** Hata mimi...sawa,bora tu usianze kuniambia mambo yako yakijinga.

**28.** **DAVID:** Mambo gani hayo Karembo? Kwani kukwambia nakupenda ni ujinga? Wewe umzuri karembo**.**

29. **KAREMBO:** Huh?**( AKIWA NA HAMAKI)** sasa huji n'goo! Kwaheri!

30. **DAVID:** Karembo!…(**PLEADING)** Karembo….

**NARRATOR:** Najuwa unalodukuduku unalotaka kulituliza kwa kuniuliza ni kwa nini karembo hataki kumsikiliza david lakini yote hayo ni maadili aliyojifunza kutoka kwa mamake kwamba siku zote ampe sikio la mbuzi mvulana yeyote atakayemkabili , hata hivyo akilini mwake alikuwa akiwaza kuhusu sura ya nduguye na haikuchukuwa muda kujua yote.

**<u>SCENE THREE: HOSPITAL ENTRANCE</u>**

**C-SFX: WIDE DOOR SWINGS OPEN, MAKING NOISE INWARDS AND OUTWARDS, PEOPLES VOICES; HOSPITAL ATMOSPHERE; STEPS**

31. **KAREMBO:** (**EXCITEDLY)**
Mama....

32. **BETTINA:** (**FAINT WEAK VOICE)**
Mbona umechelewa hivyo?

33. **KAREMBO:** Nilichelewa shule... mama hebu nimuone? oh... ni mzuri..lakini mdogoo.... angalia vikono na vidole vyake vyapendeza.

**34. D-SFX: SLIGHT CHUCKLE FROM BABY ZAWADI**

35. **KAREMBO:** Mama uko tayari kurudi nyumbani au

bado hujaruhusiwa?

36. **BETTINA:** Ndio.. daktari alisema naweza kwenda nyumbani... nisaidie hizi nguo na mimi nitambeba zawadi...

**37. E-SFX: SAME WIDE DOOR OPENS WIDE**

38. **KAREMBO:** Hebu subiri... mama, ulikuwa wajuwa kuwa unaweza kupata neti iliyotibiwa ya mbu kutoka hapa hospitali? Mwalimu wangu mkuu alinieleza leo shuleni ni muhimu kujikinga na mbu ili wasimuume zawadi na kumuambukiza malaria.

39. **BETTINA:** Sina habari mwanangu! Hata hivyo si muhimu sana.. hatujawahi kutumia neti miaka yote hiyo na kwanini tujipe hilo kero lote?

40. **KAREMBO:** Lakini mama... unajuwa jioni.. **(AKIIGA SAUTI YA MBU )** hawa mbu wote ni hatari iwapo watamuuma zawadi kivyovyote.. pia nimejifunza kuwa mbu wanapoigusa neti tu iliyotibiwa wanakufa fweee!,si huo ni ujumbe mzuri mama?

**41. BETTINA:** **(TIRED OF EXPLANATIONS)**
Ah haya sawa, waulize hao manesi hapo ntakusubiri hapa.

**42. F-SFX: SAME WIDE DOOR SWINGS OPENS AGAIN**

43. **BETTINA:** Mbona umerudi haraka? Wamesemaje?

44. **KAREMBO:** Hata! Nimewauliza nao wakanipa neti.. hii hapa..

45. **BETTINA:** Sawa! Basi twende nyumbani

46. **KAREMBO:** **(Laughing)** Haya naja

**NARRATOR:**Kuna furaha tele panapozaliwa mtoto,na kwa zawadi ilikuwa vivyo hivyo. walipofika nyumbani kwao walipokewa na shangwe na nderemo, vicheko na tabasamu kila sehemu ya eneo hilo.. Majirani wa mbali na karibu walikuja na kumbeba mtoto na kutoa pongezi kwa wazazi hao... fauka ya hayo...

**<u>SCENE FOUR: MASIKAS HOME</u>**

47. **KAREMBO:** Mama wacha nikufungie neti kabla ya kumlaza zawadi... sitaki aumwe na mbu hata mara moja...

**48. BETTINA:** (**IMPRESSED BY KAREMBO)**
Naona utakuwa mama mzuri wajua kulea wewe... lakini kwa sasa iwache hiyo kazi, nenda ukanitengezee uji.

49. **KAREMBO:** Lakini mama ni lazima tumlinde kwani wageni wetu wasioalikwa tayari wanataka damu yetu...

**50. G-SFX: BUZZING MOSQUITO SOUNDS**

51. **BETTINA:** **(FURIOUSLY)**
Mimi ndio mama hapa! Najuwa kulea watoto wangu vizuri sana.. kwa hivyo hivi sasa nenda ukafanye yale niliyokutuma! Nipikie uji na uutie limau kidogo nataka huo uchachu unitulize mate...

52. **KAREMBO:** Sawa mama...

**53. H-SFX: DOOR OPENS, MASIKA ENTERS SINGING A HAPPY SONG TO WELCOME HIS SON.**

54. **MASIKA:** **(Singing)**
Yuko wapi mfalme wa afrika! Sifa na mrithi wangu?

55. **BETTINA:** Hutaki hata kujuwa nimeshindaje? Ni wewe na mwanao tu?

56. **MASIKA:** **(ACTING SORRY)**
samahani basi mama zawadi...haya habari za leo?

57. **Bettina:** **(NOT BUYING THIS LINE)**
Hmm.. kwa siku moja tu nimetawazwa na kuitwa mamake zawadi badala ya mamake karembo? Wanaume wa kiafrika? Kwani wasichana wana makosa gani? Huoni karembo binti yako ndiye wa kwanza darasani mwao ilihali huyo david mvulana ndiye anayevuta mkia ! hata hivyo ni sawa. Zawadi ameshalala.. je una kitoweo chochote? Tumerudi sasa hivi na ningelipendelea supu ya mbuta...

58. **MASIKA:** **(TAKES DEEP BREATH)**
wapi mamake ? Samaki nikamamawalioagana! Sikushika hata kizeri kimoja licha ya samaki... neti yangu imechanika yote! Hata nasadiki samaki wananilaghai wanaponiona baharini... wakiingia wana kula chambo chote na wakitokea mashimoni... ni sarakasi

iliyonibughudhi mno!

59. **BETTINA:** Pole mume wangu.Kesho pia ni siku...

**60. MASIKA:** Kesho pia ni siku ya fedheha tena... kila siku ianzapo hujihisi duni kwani siwezi kutafutia riziki aina yangu...hii ni nini??(**TAKING HOLD OF THE UNOPENED MOSQUITO NET)**

61. **BETTINA:** Hiyo ni neti ya kujikingia mbu nilipewa hospitali.. walinipa bila malipo yeyote... itasaidia kuzuia mbu wasimuume zawadi na kumuambukiza malaria... karembo alinieleza kuwa neti hii imetibiwa na huwauwa mbu mara moja pindi waigusapo.

62. **MASIKA:** **(THOUGHTFUL)**
Hmm..zawadi amezaliwa na nguvu kama babake... watoto wangu hawahitaji mambo hayo ya kizungu... zawadi sasa ni miaka kumi na nne na hakuhitaji neti na ana afya yake nzuri tu.

63. **BETTINA:** Masika!Zawadi ana siku moja tu! Hakuna ubaya kujihadhari ... hebu nisaidie

tuitundike juu.. labda uitunge darini... na hapa naona kuna maelezo ya kuitumia...

64. **MASIKA:** Hakuna shida,kwanza nataka nishibe ndio nipate nguvu.

**65. BETTINA:** **(SARCASM)**
Nilifikiria ulisema kuwa una nguvu.. (**LAUGHS)**

66. **MASIKA:** Usinidhihaki zaidi,nimekuwa na siku mbaya tayari.

**67. J-SFX: MORE MOSQUITO BUZZING SOUNDS.**

68. **BETTINA:** Haya basi tafadhali funga hilo dirisha hao mbu walioingia wanatutosha...

**69. K-SFX: Some rustling of cloth WOODEN WINDOW CLOSES WITH BANG**

**<u>OUTRO/NARRATOR:</u>**

Masika akifunga dirisha nasi tunakifunga kipindi chetu cha pili kuhusu malaria katika hadithi**"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA JAMII DHIDI YA MALARIA**" lakini Masika anapanga nini anapoiona neti ya kuzuia mbu? Niyapi yatakayompata

karembo baada ya kuumwa na mbu? Ili ujifunze mengi na ujuwe zaidi yaliyotokea jiunge nasi wiki ijayo  na usisahau kutuma maoni yako au hoja zako au unapotaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti www.dw-world.de/lbe.

Hadi wakati mwengine.kwaheri.